

**Kutoka Katika Kutokuwa na Umoja Uadi
Katika Umoja
(From Disunity to Unity)**

Na

John Kombo

Kutoka Katika Kutokuwa na Umoja Uadi Katika Umoja

Na

John Kombo

June 20, 2014

Kutoka Katika Kutokuwa na Umoja Uadi Katika Umoja

Je kuna uwezekano kutoka katika “KUTOKA KATIKA KUTOKUWA NA UMOJA HADI KATIKA UMOJA?”

Tunaposikiliza taariza za habari katika redio zetu, na kutazama runinga zetu na kusoma magazeti yetu yanayotuzunguka, tunaona kile ambacho dhambi hufanya katika ulimwengu wetu. Mataifa hupigana vita, makabila na waatawala upigana kila mmoja; ndoa uharibika, nyumba nyingi huvunjika. Watoto huzaliwa na kucheza pamoja. Lakini nini hutokea baadae? Wanakuwa wakiwachukia kila mmoja wao na kutengana kama wazazi wao. Kati ya kila mtu mzima vita huibuka, na mara nyingi tamaa mbaya huondoa mema. Mkanganyiko na mvutano huishia kwa kuchana kila mmoja na jamii kutengana. Kila unachokiona karibu yako, izidishe na kile kilichotokea katika ulimwengu mzima. Na ufikirie kuhusu kile ambacho macho ya kimwili hakiwezi kuona – vita ya kiroho katika ulimwengu wa kimbingu. Alafu tunaweza kujua hali ni hatari kiasi gani.

Matukio hapo juu ni matokeo ya uongozi ulioanguka, iwe kibinadamu au kishetani. Iwe katika kanisa au nje ya kanisa. Wanadamu ndio viongozi wa ulimwengu (Mwa. 1:26, 28; Zab. 8:4-6). (Machafuko na ghasia vilianza dhambi ilipoingia, na imeendelea toka kipindi hicho). Mungu alipoviumba vitu vyote, “*Ilikuwa nzuri*” (Mwa. 1:31). Hivyo utawala wa mwanadamu unapaswa kusaidia kutimiza maelezo, “*Ilikuwa nzuri?*” dhambi utawala mwanadamu uongoza. Dhambi katika utawala, ukabidhi utawala kwa Shetani. Nini kinaendelea leo kulingana na taarifa ya jinai, vita, na ukandamizaji mbaya tunaousoma katika magazeti inaweza kusema vizuri “*ilikuwa mbaya sana*”.

“Taarifa Njema” Mungu amewaopa wanadamu wapya Yesu Kristo ambaye dhambi yake hurudisha mgawanyiko wa dhambi. Mungu amemweka enzi kama aliye kichwa ambaye Mungu anaweza, “*kuleta vitu vyote vya mbinguni na duniani pamoja*” (Efe. 1:10). Yesu Mwana wa Mungu anatawala hadi atakapowaangamiza maadui zake wote. Tunafahamu, tayari wakati maadui zake wanashauku kubwa, yeye anafanya kazi kubwa ya kutawala. Anauwezo wa kumbadilisha mwenye dhambi na kuwakusanya pamoja kama familia moja yenye upendo, “*Mwili mmoja*” (Efe. 2:16; 3:6; 4:4, 25; Kol. 3:15). Sisi ni washirikaa katika mwili huu na tunatoka katika mataifa yote (Mat. 28:18-19; Ufu. 5:9; 7:9). Hata yale mataifa ambayo ni maadui dhidi ya nyingine, wazazi

ambao ni maadui dhidi ya wenzao, n.k.; washirika wa mwili huu tu, kanisa ambao, wanaitwa Wakristo (Mdo. 11:26), *“Ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha na kuomba, na kunifuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi zao, na kuiponya nchi yao.”* (2 Nya. 7:14).

Wakristo kila mahali, huu ni wakati wa kuungana katika upendo wa Bwana wetu pekee Yesu Kristo na kuombea kile kinachotokea ulimwenguni mwote. Tunasikia kuhusu Al-Shabab, Boko Haram, kutaja mtazamo. Raia mwema anayependa amani wanaogopa na mara nyingi uhofia maisha yao.

Ninaishi Kenya; ninaipenda nchi yangu na watu wote. Ninachukia ukabila, ambayo kwa miaka mingi imeigawanya nchi yetu kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kama Mkristo ni maombi yangu kwamba siku moja Mungu Baba yetu, atashuka chini na kuleta umoja unaohitajika ili tuishi pamoja katika amani. Watumishi wote wa Mungu pia wawe na umoja katika kuhubiri amani kwa watu. Yesu mwenyewe katika sala yake, aliomba, *“Wala si hao tu ninaowaombea lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja, kama wewe Baba ulivyo ndani yangu, nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetuili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.”* (Yoh. 17:20-21)

Mungu aibariki familia yake katika Ulimwengu. Hili ni Kanisa la Kristo.

John Kombo

Kanisa la Kristo Baruti

Nakuru, Kenya

